



## *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

### **1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 DISEMBA, 2023 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11- 20 DISEMBA, 2023**

#### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 DISEMBA, 2023**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo katika kizio cha kaskazini (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii iliendelea kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuwepo katika maeneo ya nchi yetu. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi. Hali hii ilichangia kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu.

#### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01- 10 DISEMBA, 2023**

Viashiria vya hali ya hewa vya hapo juu vilipelekea baadhi ya maeneo ya nchi yetu kupata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi hasa kwa baadhi ya maeneo ya pwani ya kaskazini, nyanda za juu kaskazini mashariki, maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, ukanda wa Ziwa Viktoria na magharibi mwa nchi. Hata hivyo, vipindi vya mvua nyepesi hadi mvua za wastani viliripotiwa katika maeneo ya Kati mwa nchi, kusini na maeneo ya pwani ya kusini.

### **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 DISEMBA, 2023**

#### **2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 DISEMBA, 2023**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuwepo katika maeneo ya nchi yetu. Joto la bahari la juu kidogo ya

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

wastani linatarajiwa katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa kuwepo katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu.

## **2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 DISEMBA, 2023**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo vinatarajiwa.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua na ngurumo za radi zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa.

Imetolewa na;

### **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)